



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

### TAARIFA KWA UMMA

Dar es-Salaam 23 Oktoba, 2020

Tume ya Taifa ya uchaguzi inaendelea na maandalizi ya uchaguzi katika hatua za mwisho, zikiwa zimebakia siku nne kabla ya siku ya kupiga kura yaani tarehe 28 Oktoba.2020.

Katika kipindi hiki Tume imebaini kuwepo kwa kundi la watu wakiwemo baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa ngazi ya juu ambao wamejipanga kuharibu taswira ya uchaguzi, kwanza wamejipanga kueneza taarifa za uzushi na uongo na tayari wameanza. Pili wamejipanga kutafuta na kuweka vielelezo vya uongo na visivyo na uhalisia wakivihusisha na michakato ya uchaguzi huu, kwa lengo la kuleta taharuki kwa wadau wa uchaguzi na wananchi kwa ujumla.

Tume imefanikiwa kunasa mojawapo ya majadiliano hayo katika group la wanaojiita fichua Tanzania ambayo wameonesha kujipanga kukubaliana kufanya propaganda kutoa taarifa za uongo.

Mojawapo ya mipango ya kuzusha ni wimbi linaloendea la kudai kwa uwepo wa vituo hewa natolea mfano Jimbo la Misungwi. Jimbo hilo lina kata 27 na vituo vilivyotumika kuandikisha wapiga kura ni 291 ina vituo vya kupiga kura 549. Hivi karibuni wazushi walisema ni vituo 470, mbapo idadi ya wapiga kura katika kila kituo haitakiwi kuzidi 500 na jimbo hilo la misungwi lina wapiga kura 193,294.

Kama walivyojipanga hali hii ya kudai vituo hewa inaendelea kujitokeza katika maeneo mbalimbali. Nawasihi wananchi mpuuzie taarifa hizo kwani Zoezi la uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lilifanyika kwa uwazi na wadau wa uchaguzi walishirikishwa katika hatua zote.

Vyama vya Siasa tayari vimepatiwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na orodha ya vituo vya kupiga kura 80155 nchi nzima. Vituo hivyo ndivyo vitakavyotumika kupiga kura siku ya uchaguzi na si vinginevyo.

Ikumbukwe vyama vya siasa vilipatiwa orodha ya wapiga kura kwa ajili ya kutafuta wadhamini mikoani ili kutimiza masharti ya uteuzi, ambapo hatukuwasikia wakizungumzia wapiga kura hewa miongoni mwa waliowadhamini .


Uzushi mwingine wenye nia ovu ya kuleta taharuki kwa wananchi katika kipindi hiki, ni sehemu ya video inayoonesha kuwapo kwa gari lililobeba masanduku ya kura. Wadau na wananchi tunapaswa kujiuliza maswali kadhaa kabla ya kuamini hicho kilichokusudiwa kwa mfano, hapo lipopokutwa gari hilo ni eneo gani katika nchi hii, namba ya gari, ndani ya masanduku hayo kuna nini, kama ni karatasi za kura zinawahusu wagombea gani na ziko katika hali gani.

Tume inapenda kuwafahamisha wadau na wananchi kwa ujumla kuwa masanduku hayo hayahusiani na uchaguzi wa mwaka huu kwani namba zilizopo kwenye masanduku hayo sio zenyewe na hata rangi ya lakiri iliyotumika katika masanduku hayo siyo itakayotumika katika uchaguzi huu hivyo wajipange upya.

Tume inasikitishwa na vitendo hivyo vya uzushi na inatoa onyo kwa wale wote wanaondelea na uzushi kwa nia ovu ya kuharibu uchaguzi na haitasita kuwa chukuliwa hatua za kisheria kwa

kuwa huo ni uchochezi unaoweza kusababisha uvunjifu wa Amani.

Kwa mara nyingine nitumie fursa kutoa rai wananchi kuupuzia taarifa kama hizo kwani hazina nia njema katika kipindi hiki ambapo watanzania wanajiandaa kuchagua viongozi wanaowataka .



Dkt. Wilson Mahera Charles

**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**